



MWALIKO WA MAOMBI MAPYA NA UPANDISHAJI DARAJA WA LESENI ZA MAUDHUI (UTANGAZAJI WA KIBIASHARA – REDIO)

1. Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) ni taasisi ya Serikali iliyoanzishwa chini ya Sheria ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania Na.12 ya mwaka 2003 ili kusimamia mawasiliano ya kielektroni na huduma za posta katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na huduma za utangazaji kwa upande wa Tanzania Bara.
2. Kwa mujibu wa Kanuni za Taratibu za Utoaji Leseni, Tangazo la Serikali Na.422 la mwaka 2014, TCRA imeainisha Masafa kwa ajili ya utoaji wa Huduma za Maudhui. Hivyo dirisha la maombi ya leseni ya utoaji wa huduma za maudhui ya radio (Matangazo ya Kibiashara – Redio) limefunguliwa katika maeneo yafuatayo:-

Mkoa	Eneo la Huduma	Kiasi cha Masafa Yaliyopo
Mwanza	Mwanza	5
Dodoma	Dodoma	2
Arusha	Arusha	3
Njombe	Njombe	2
	Ludewa	2
	Wanging'ombe	2
	Makete	2
	Makambako	2
Kagera	Kyerwa	1
	Missenyi (Mutukula)	1
	Biharamulo	1
Kigoma	Buhigwe	1
	Kigoma	1
	Kasulu	3
Geita	Mji wa Geita	1
	Chato	1
	Bukombe	1

Mkoa	Eneo la Huduma	Kiasi cha Masafa Yaliyopo
Shinyanga	Mji wa Kahama	1
	Kishapu	2
	Manispaa ya Shinyanga	1
Simiyu	Bariadi	2
	Busega	2
	Itilima	2
Mtwara	Mtwara	2
	Masaki	2
	Tandahimba	2
	Newala	2
Singida	Manispaa ya Singida	2
	Manyoni	1
	Ikungi	1
	Mkalama	1
	Iramba	1
Rukwa	Manispaa ya Sumbawanga	2
	Sumbawanga Vijijini	2
	Kalambo	2
	Nkasi	2
Manyara	Hanang	2
	Kiteto	2
	Mbulu	2
	Simanjiro	2
Ruvuma	Mbinga	1
	Nyasa	1
	Tunduru	1
	Manispaa ya Songea	2
	Namtumbo	1
Lindi	Nachingwea	1
	Kilwa	1
	Mtama	1
	Liwale	1
	Mji wa Lindi	2
	Ruangwa	2
Morogoro	Mvomero (Turiani)	1
	Ifakara	1
	Gairo	1
Tanga	Kilindi/Tanga	1
	Mkinga	1
Mara	Mji wa Musoma	1
	Rorya	1
	Mugumu	2
	Tarime	1
Iringa	Manispaa ya Iringa	1
	Kilolo	1
	Mafinga (Mufindi)	1
Tabora	Manispaa ya Tabora	2

Mkoa	Eneo la Huduma	Kiasi cha Masafa Yaliyopo
	Igunga	1
	Kaliua	1
	Urambo	1
	Nzega	1
Katavi	Mpanda	2
	Nsimbo	2
	Tanganyika	2
	Mlele	2

3. Waombaji wanatakiwa kuzingatia mwongozo wa uwasilishaji wa maombi unaopatikana katika tovuti ya TCRA: <https://www.tcra.go.tz/uploads/documents/sw-1665384791-Mwongozo%20kwa%20Waombaji%20-%20ITA%207%20Oktoba%202022.pdf>
4. Maombi yote ya utoaji wa huduma tajwa hapo juu yawasilishwe kwa kupitia mfumo wa maombi ya leseni wa TCRA uitwao **Tanzanite Portal** kupitia kiunganishi kifuatacho: <https://tanzanite.tcra.go.tz/index.htm> kabla ama ifikapo tarehe 12 Novemba, 2022.
5. Tafadhali zingatia kwamba, endapo waombaji katika eneo fulani la huduma wako wengi zaidi ya kiasi cha Masafa yaliyoainishwa katika eneo hilo, **TCRA itaweka Masafa ya eneo husia katika mchakato wa ushindani, yaani zabuni / Mnada.**
6. Waombaji watakaoingia kwenye **mchakato wa ushindani wa zabuni au mnada watajulishwa ili waweze kuwasilisha zabuni zao katika bahasha iliyofungwa ambayo itafunguliwa mbele ya wazabuni wote.**

Imetolewa na:

Mkurugenzi Mkuu,
Mamlaka ya Mawasilaino Tanzania,
Mawasiliano Towers,
20 Barabara ya Sam Nujoma,
S. L. P. 474,
14414 DAR ES SALAAM.